# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI


MKOA WA ARUSHA
MAWASILIANO YOTE KWA
MKUU WA SHULE
SIMU: 0752 291 852
0621 570 852

S. L. P. 83,
MTO WA MBU,
MONDULI.
ARUSHA.
…………………..


KUMB. NA. RSS/FOS/SEC.2
JINA LA MWANAFUNZI
……………………………………………..
……………………………………………...
………………………………………………

YAH: MAAGIZO YA MWANAO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RIFT VALLEY KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

UTANGULIZI

Nafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2024. Shule ya Sekondari Rift Valley ipo umbali wa kilometa 130 kutoka Arusha mjini. Usafiri wa basi kutoka Arusha mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Arusha mjini nauli Tsh 6,000/= kwa hiace na Tsh 6,000 kwa mabasi makubwa na Tsh 7,000/= kwa noah. Shule ipo katika mji mdogo wa Mto wa mbu (kituo cha kushukia ni stendi ya karatu Mto wa mbu kama unatoka Arusha) Shule ipo umbali wa kilometa 5 kutoka barabara kuu ya Arusha, unaweza kufika shuleni kwa kutumia usafiri wa Bajaji Tsh 10,000/= na pikipiki Tsh 3,000/=

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **08/01/2024** unatakiwa kuripoti shuleni kuanziatarehe **08/01/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2024** hakikisha unaripoti shule ndani ya siku **14** tangu shule kufunguliwa.Mwanafunzi asiporipoti mzazi/mlezi atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata Elimu.Aidha iwapo utampeleka mtoto wako **shule binafsi** toa taarifa mapema kwa **mkuu wa shule** au katika ofisi ya **Afisa elimu sekondari** ili kuepuka usumbufu.

## 2.**0** **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.0 Sare za shule

Sare ya shule ni rangi ya **DARK BLUE**

**WAVULANA**

a) **Sare ya darasani**: Suruali mbili za rangi ya **DARK BLUE** zenye marinda mawili,na zenye upana wa kutosha na zenye pindo chini (**TURN UP),**mashati mawili meupe ya mikono mifupi, soksi nyeusi pea mbili, sweta la DARK BLUE shingo V, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba.

b) **Sare ya kushindia**: Suruali mbili za **rangi nyeusi,** T-shirt ya **rangi nyekundu** yenye kola **isiyokuwa na maandishi wala picha.**

**WASICHANA**

a) **Sare ya darasani**: Sketi mbili za rangi ya **DARK BLUE** zenye marinda ya kawaida **ndefu zinazofika kwenye vifundo vya miguu,** mashati mawili rangi nyeupe ya mikono mifupi, soksi ndefu nyeupe za kuvuka magoti, sweta la rangi ya **dark blue** yenye shingo V na kiatu cheusi cha kufunga kamba cha **ngozi kisichokuwa na kisigino.**

**b) Sare ya kushindia**: Sketi ya rangi nyeusi yenye marinda ya kawaida,ndefu inayofika kwenye vifundo vya miguu,T-shirt rangi nyekundu yenye kola **isiyo na maandishi wala picha.**

**KWA WASICHANA WA KIISLAMU WASHONE (LAZIMA)**

**SARE YA DARASANI**: Sketi mbili ndefu na pana za **dark blue zinazofika kwenye vifundo vya miguu,** short kanzu nyeupe mbili za **mikono mirefu** pana na ndefu hadi kwenye magoti, jalabibi leupe la kushona lifunike mikono (**la dukani haliruhusiwi).**

**SARE YA KUSHINDIA**:Sketi ya rangi nyeusi yenye marinda ya kawaida,ndefu inayofika kwenye fundo za miguu,short kanzu nyeupe moja ya mikono mirefu na pana.

WANAFUNZI WOTE WANATAKIWA WAJE NA MAHITAJI YAFUATAYO:

- Godorola **TANFOAM** futi mbili na nusu (aina nyingine ya godoro haitapokelewa hii ni ili kuepuka usumbufu wa kununua godoro kila mara), mto, chandarua, mashuka mawili **rangi ya Pink kwa wasichana** na **rangi ya blue kwa wavulana**, mswaki, Sanduku la bati imara na kufuli yake, tochi, dawa ya meno, mafuta ya kujipaka, sabuni, vyombo vya kulia chakula (sahani, kikombe, vyote vya bati na kijiko), malapa ya tairi yanafaa zaidi, nguo za ndani za kutosha, kitana, madaftari makubwa 10 au zaidi, kalamu na pensel, mathematical table (four figure) begi la madaftari, rangi nyeusi ya viatu (KIWI), brash ya viatu na blanketi **sio maasai shuka.**
- Kwa wasichana, raba za michezo za mtumba, track suit nyekundu, t-shirt rangi nyekundu yenye shingo ya mviringo na soksi ndefu za michezo rangi nyekundu na **ndoo ndogo mbili.**
- Kwa wavulana Truck suit nyekundu,T-shirt nyekundu yenye shingo ya mviringo na Bukta nyekundu,Raba za michezo za mtumba,Soksi nyekundu ndefu, **na ndoo ndogo mbili**
- **Kamusi ya Kiswahili sanifu.**
- **Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza** ni lazima kwa kila mwanafunzi kuja nayo. (**ADVANCED LEARNERS DICTIONARY )**
- **Bunda moja la K**aratasi ya **RIM**

- **Jembe 1 na mpini wake.**

**2:2<u>SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII</u>**

1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-
2. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla nijambo la lazima.
3. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
4. Kutimiza maandalio ya jioni(Preparation).
5. Kuwahi katika kila shughuli na nyingine utakazopewa.
6. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa Uanafunzi wako katika shule hii.
7. Kutunza usafi wa mwili na mazingira.
8. Kuvaa sare za shule wakati wote.
9. Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vya dini kwa Imani yake.
10. Kila wiki ya mwisho wa mwezi mzazi/mlezi fika shuleni kufuatilia maendeleo ya taaluma ya mwanao(Ni vizuri kufika siku za kazi walimu wakiwepo)

2:3 **<u>MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE:-</u>**

i) Wizi
ii) Uasherati na Ushoga
iii) Ubakaji
iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya Kulevya kama vile uvutaji wa bagi,kokeni,mirungi au kuberi nakadhalika.
v) Kupigana na Kupiga.
vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii) Kudharau bendera ya Taifa
viii) Kuoa au Kuolewa
ix) Kupata mimba ua Kuharibu mimba,au Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
x) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
xi) Kukataa adhabu kwa makusudi
xii) Mwanafunzi kumiliki simu au laini ya simu ni marufuku

**<u>AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MALEZI YA MWANAE</u>**

**<u>(ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi na kuiwasilisha shuleni)</u>**

Mimi.......................................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……...............................................................ninaahidi kumhudumia mwanangu na kumpatia mahitaji yake kwa wakati na kushirikiana na shule kumlea mtoto huyu. Aidha ninaahidi kwamba nitahakikisha mwanangu atasoma na kumaliza shule na hivyo sitakubaliana na utoro wa aina yoyote.

Nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu kama ni **wakike** hatapata ujauzito wala sitamuoza au kupokea mahari wakati wote wa masomo yake. Endapo nitakiuka ahadi hii hatua kali za sheria zichukuliwe dhidi yangu

Saini ya Mzazi/Mlezi: ..................................................Tarehe: ……………………

<u>Mawasiliano</u>:

Namba ya Simu: 1………………………………………………………..

2…………………………………………………….

**<u>AHADI YA MWANAFUNZI KUHUSU KUFUATA SHERIA ZA SHULE</u>**
**<u>(ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)</u>**

Mimi ………………………………………. ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha…………..2024 ninaahidi kwamba, nitafuata sheria , kanuni na taratibu za Shule na kutoshiriki kwenye migomo niwapo shuleni; nikienda kinyume na Sheria hizo nichukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria husika niliyoivunja/kiuka.

Saini ya mwanafunzi: ……………………………….. Tarehe: ………………….

**……………………..**

**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**
**SHULE YA SEKONDARI RIFT VALLEY**

**TAARIFA YA MWANAFUNZI – KIDATO CHA ………………. MWAKA ………………**

1. Shule ya Msingi aliyotoka: ………………………………………………………………..
2. Jina la mwanafunzi: …………………………………………… Jinsia: Me ……. Ke ……
3. Tarehe ya Kuzaliwa: ………………………………………………………………………
4. Namba ya Usajili: ……………………………………………………………………….
5. Kijiji atokacho: ………………………………………………………………………….
6. Kata atokayo: …………………………………………………………………………..
7. Mwenyekiti wa kijiji au Serikali ya Mtaa atokako: ………………………………………
   Namba ya Simu ya mwenyekiti ……………………………………………………………
8. Jina la Balozi atokako: ……………………………………………………………….…
   Namba ya Simu: ………………………………………………………………………..
9. Jina la Baba/Mlezi: …………………………………………………………………….
   Namba ya Simu: ……………………………………………………………………….
10. Jina la Mama/Mlezi: ……………………………………………………………………..
    Namba ya Simu: ………………………………………………………………………
11. Jina la ndugu wa karibu:
    (i) Jina la ndugu: 1 …………………………………………………………………….
        Namba ya Simu: …………………………………………………………………...
    (ii) Jina la ndugu 2: ……………………………………………………………………
        Namba ya Simu: …………………………………………………………………..
    (iii) Jina la ndugu 3: …………………………………………………………………...
        Namba ya Simu: ……………………………………………………………………

**Ninathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi.**

**Jina: ………………………………………… Saini: ………………… Tarehe: ………………**

Mkuu wa shule**: …………………………. Saini: ……………………. Tarehe: ………………**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**RIFT VALLEY SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer(government Hospital) in respect of all new student to the School.

Student's name: ……………………………………………………………………………………

Blood count (red or white): ……………………………………………………………………………….

Stool examination: ………………………………………………………………………………..….

Urine analysis: ……………………………………………………………………………………………….

Syphilis: ……………………………………………………………………………………………..….

T.B. Test: ……………………………………………………………………………………………………

Eye Test: …………………………………………………………………………………………...….

Ears Test: ……………………………………………………………………………………….….

Chest: ……………………………………………………………………………………………....

Liver: ……………………………………………………………………………………………….

Abdomen: ………………………………………………………………………………………………
(Pregnancy test for girls)

Any other physical defect: ………………………………………………………………………….

Date: ……………………………………….

Signature: ……………………………………

Designation: …………………………………

Station: ………………………………………

Stamp: